Mbiu ya
VIPIMO
TOLEO NA .003
JARIDA LA WAKALA WA VIPIMO (WMA)
JANUARI - APRILI, 2025

# RAIS SAMIA APONGEZWA KUWEZESHA UJENZI OFISI KUU WMA




HABARI UK. 3

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan

# WAZALISHAJI BIDHAA ZA VIWANDANI MMEMSIKIA MHESHIMIWA WAZIRI?!

Moja ya habari katika Toleo hili ni kuhusu maelekezo ya Waziri wa Viwanda na Biashara, Mhe. Dkt. Selemani Jafo kwa wazalishaji wa nondo na bati hapa nchini kutengeneza bidhaa zenye ubora na zinazokidhi viwango vilivyowekwa kisheria ili Watanzania wanaonunua bidhaa hizo wapate mali halisi kulingana na thamani ya fedha wanazolipa.

Mheshimiwa Waziri amekemea baadhi ya wafanyabiashara ambao wamekosa uaminifu kiasi cha kuzalisha bidhaa zilizo chini ya kiwango ambapo amesema zinaathiri majengo ya wale wanaozinunua na kuzitumia.

Tunawakumbusha na kuwasisitiza wafanyabiashara wa aina hiyo wasio waaminifu kuacha mara moja tabia hiyo. Tunawataka kufanya kazi yao kwa kuzingatia sheria na miongozo iliyopo. Sisi Wakala wa Vipimo hatutasita kumchukulia hatua za kisheria yeyote atakayebainika kufanya udanganyifu kwa kuzalisha bidhaa za ujenzi au nyingine zozote zilizo chini ya kiwango.

Wataalamu wetu wamekuwa wakiendesha kaguzi katika sehemu mbalimbali kote nchini ili kuhakikisha bidhaa zote zinazozalishwa kwa ajili ya matumizi katika sekta mbalimbali zinakidhi vigezo na viwango.

Lengo la kuendesha kaguzi hizo ni kuwalinda walaji kwa kuhakikisha kwamba siyo tu wanapata bidhaa sahihi kulingana na thamani ya malipo wanayotoa bali pia ni kuikinga na kuilinda jamii dhidi ya matumizi ya bidhaa zilizo chini ya viwango ambazo zinaweza kuhatarisha usalama wa wananchi.

Enyi wafanyabiashara msio waaminifu, tunaamini mmemsikia Mheshimiwa Waziri na hamtathubutu tena kutengeneza bidhaa zilizo chini ya viwango. Kila mmoja achape kazi kwa uaminifu pasipo kuhatarisha usalama wa wananchi. Wakaidi tutawabaini na tutawawajibisha.

Mbiu ya VIPIMO
JARIDA LA WAKALA WA VIPIMO (WMA)

BODI YA UHARIRI

MWENYEKITI
Alban Kihulla

MHARIRI MSAIDIZI
Paulus Oluochi

WAJUMBE
Karim Mkorehe
Francis Olwelo

WAANDISHI
Veronica Simba
Paulus Oluochi

MHARIRI MKUU
Veronica Simba

MSANIFU KURASA
Lucas Gordon

## KATUNIKA KI-VIPIMO



# RAIS SAMIA APONGEZWA KUWEZESHA UJENZI OFISI KUU WMA

**Dodoma**

Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Dkt. Hashil Abdallah amempongeza na kumshukuru Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kuwezesha ujenzi wa Jengo la Ofisi Kuu ya Wakala wa Vipimo (WMA) jijini Dodoma akisema ni matumizi mazuri ya fedha za Watanzania.

Aliyasema hayo Januari 20, 2025 baada ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa Jengo hilo ambalo limegharimu shilingi bilioni 6.2 na liko katika hatua za mwisho kukamilika.

Akizungumza na Waandishi wa Habari, Dkt. Abdallah alisema kuwa lengo la ujenzi wa jengo hilo ni kuhakikisha utoaji huduma katika sekta ya biashara hususan katika bidhaa zinazotoka viwandani unaboreshwa.

Akifafanua, alisema kuwa maboresho ya kutoa huduma bora katika sekta ya biashara na katika uendelezaji wa viwanda ni pamoja na kuwa na mazingira mazuri kwa wafanyakazi na yale ya utoaji wa huduma hizo.

"Na katika hili, Dkt. Samia Suluhu Hassan amefanya mambo mengi makubwa, mojawapo ikiwa ni ujenzi wa jengo hili ambalo tunakwenda kulizindua hivi karibuni," alisisitiza.

"Ninyi wenyewe ni mashahidi; fedha za Watanzania zinaenda kukamilisha ujenzi huu ili tuweze kutoa huduma bora katika jamii ya wafanyabiashara na tuweze kuleta maendeleo na tija katika sekta ya viwanda," aliongeza Katibu Mkuu.

Kwa upande wake, Afisa Mtendaji Mkuu wa WMA, Alban Kihulla, pamoja na kuunga mkono pongezi na shukrani kwa Rais Samia kuwezesha ujenzi wa jengo hilo, pia alibainisha kuwa kukamilika kwake siyo tu kutaboresha mazingira ya wafanyakazi wa Wakala bali pia kwa Serikali kwa ujumla.

Akidadavua baadhi ya faida zitakazopatikana kutokana na kukamilika kwa jengo hilo, Mtendaji Mkuu alieleza kuwa maabara ya kisasa ndani yake itawezesha kuhifadhi vifaa ambavyo kitaalamu vinajulikana kama vyenye usahihi wa kati au kwa lugha ya kigeni 'secondary standards'



*Katibu Mkuu Wizara ya Viwanda na Biashara, Dkt. Hashil Abdallah akizungumza na waandishi wa habari baada ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa Jengo la Ofisi za Makao Makuu ya Wakala wa Vipimo (WMA), eneo la Medeli jijini Dodoma, Januari 20, 2025.*

"Niwakumbushe tu kuwa, Wakala wa Vipimo ndiyo umepewa jukumu la kuhifadhi vipimo vyenye usahihi wa kati, kwa maana pale ndiyo tunalinganishwa kimataifa na ndipo unaleta ongezeko la imani kwa wawekezaji kuja kuwekeza nchini wakijua kwamba usahihi wa vipimo unafuatiliwa kutoka ngazi ya mfanyabiashara mpaka ngazi ya kimataifa."

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, mwakilishi wa Mkandarasi anayejenga jengo hilo kutoka Kampuni ya Mohamed Builders, Bwana Burhan Hamza pamoja na Mshauri Elekezi kutoka Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST), Bi Rachel Lista walithibitisha kuwa jengo litakamilika kwa na kukabidhiwa kwa WMA hivi karibuni.

Ujenzi wa Jengo la Ofisi Kuu ya Wakala wa Vipimo, lililopo eneo la Medeli jijini Dodoma ulianza Julai 2, 2022 na matarajio ilikuwa likamilike Desemba 30, 2024 lakini Mkandarasi aliomba kuongezewa muda kutokana na changamoto ndogondogo alizokutana nazo.

Hadi sasa Mkandarasi amelipwa jumla ya shilingi bilioni 5.8 kati ya shilingi bilioni 6.2 ambayo ni gharama ya utekelezaji wa Mradi huo.

# HABARI KATIKA PICHA







*Katibu Mkuu Wizara ya Viwanda na Biashara, Dkt. Hashil Abdallah akikagua maendeleo ya ujenzi wa Jengo la Ofisi za Makao Makuu ya Wakala wa Vipimo (WMA), eneo la Medeli jijini Dodoma, Januari 20, 2025.*




*Afisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Vipimo (WMA), Alban Kihulla akitoa taarifa kwa waandishi wa habari kuhusu maendeleo ya mradi wa ujenzi wa jengo la Ofisi za Makao Makuu ya WMA jijini Dodoma, wakati wa ziara ya Katibu Mkuu Wizara ya Viwanda na Biashara, Dkt. Hashil Abdallah kukagua jengo hilo, Januari 20, 2025.*







*Taswira ya jengo la Ofisi za Makao Makuu ya Wakala wa Vipimo (WMA) jijini Dodoma. Taswira hii ilichukuliwa wakati wa ziara ya Katibu Mkuu Wizara ya Viwanda na Biashara, Dkt. Hashil Abdallah kukagua maendeleo ya ujenzi wa jengo hilo, Januari 20, 2025.*

# WAZIRI JAFO AWATAKA WAZALISHAJI WA NONDO NA BATI KUZINGATIA UBORA

**Kibaha, Pwani**

Waziri wa Viwanda na Biashara, Mhe. Dkt. Selemani Jafo amewaagiza wazalishaji wa nondo na bati hapa nchini kutengeneza bidhaa zenye ubora na zinazokidhi viwango vilivyowekwa kisheria ili Watanzania wapate mali halisi kulingana na thamani ya fedha wanazolipa.

Aliyasema hayo Februari 20, 2025 Kibaha mkoani Pwani wakati wa hafla ya kukabidhi magari matano kwa Wakala wa Vipimo (WMA) ikiwa ni sehemu ya kuendelea kuboresha utoaji wa huduma za uhakiki na ukaguzi wa vipimo.

Alisema kuwa bado kuna wafanyabiashara wanazalisha nondo zilizo chini ya kiwango ambapo matokeo yake wananchi wanaozinunua na kuzitumia bidhaa hizo, majengo yao yanakuwa hatarini.

"Kuna watu, badala ya kuzalisha nondo yenye milimita 16 anatengeneza yenye milimita 15 na sentimita kadhaa na yenye milimita 14 inakuwa chini ya milimita hizo."

Kutokana na hali hiyo, Dkt. Jafo aliielekeza WMA kuendelea kufanya kaguzi za kushtukiza kwenye viwanda vya uzalishaji wa nondo na mabati ili kuhakikisha bidhaa zinazofika kwenye masoko zinakuwa na vipimo sahihi kwa lengo la kuwalinda wanunuzi wa bidhaa hizo.

Kuhusu magari aliyokabidhi, Waziri Jafo alielekeza yakatumike katika kaguzi mbalimbali za bidhaa zilizofungashwa kwa kuhakikisha vipimo vinakuwa sahihi hususani katika nondo na mabati ili mnunuzi apate bidhaa inayoendana na thamani ya fedha anayolipa.



*Waziri wa Viwanda na Biashara Dkt. Selemani Jafo akizungumza na waandishi wa habari baada ya kukabidhi magari matano kwa Wakala wa Vipimo (WMA), Kibaha mkoani Pwani, Februari 20, 2025. Pamoja naye ni Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya WMA, Prof. Eliza Mwakasangula.*

Kwa upande wake, Afisa Mtendaji Mkuu wa WMA, Alban Kihulla, alimshukuru Waziri kwa kukabidhi magari hayo ambayo alisema yatasaidia kufika katika maeneo mbalimbali kwa ajili ya kutoa huduma za usimamizi na ukaguzi wa vipimo.

"Mhe. Waziri, leo tunajivunia sana kupata magari haya kwa maana yatatusaidia kwanza kufanya ukaguzi wa vipimo katika kipindi chote cha mwaka, lakini pia kuwafikia wateja katika sehemu kubwa, na hasa katika sehemu tulizokuwa tunashindwa kufika," alieleza Mtendaji Mkuu.

Thamani ya magari yaliyokabidhiwa ni zaidi ya shilingi bilioni moja (1,004,739,000). Magari mengine mawili yanatarajiwa kukabidhiwa kwa WMA hivi karibuni ili kuboresha utendaji kazi.




*Waziri wa Viwanda na Biashara Dkt. Selemani Jafo (katikati) akikata utepe kabla ya kukabidhi magari matano kwa Wakala wa Vipimo (WMA), Kibaha mkoani Pwani, Februari 20, 2025. Kushoto ni Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya WMA, Prof. Eliza Mwakasangula na kulia ni Afisa Mtendaji Mkuu wa WMA, Alban Kihulla.*



*Waziri wa Viwanda na Biashara, Dkt. Selemani Jafo akisalimiana na baadhi ya Wajumbe wa Menejimenti ya Wakala wa Vipimo (WMA) alipofika kukabidhi magari kwa Wakala hiyo, Februari 20, 2025 Kibaha, mkoani Pwani.*









*Matukio mbalimbali siku Waziri wa Viwanda na Biashara, Dkt. Selemani Jafo, alipokabidhi magari matano kwa Wakala wa Vipimo (WMA), Februari 20, 2025 Kibaha mkoani Pwani.*

# WIZARA YA FEDHA 'YAWANOA' WAHASIBU WMA




*Mkurugenzi wa Huduma za Biashara kutoka Wakala wa Vipimo (WMA), Karim Mkorehe (mbele-katikati), akiwa katika picha ya pamoja Wahasibu kutoka mikoa 31 ya kivipimo kote nchini baada ya kufunga mafunzo ya uandaaji wa taarifa za fedha kwa kutumia Mfumo wa Uhasibu Serikalini maarufu kama MUSE, Februari 21, 2025 mjini Morogoro.*

**Morogoro**

Wizara ya Fedha imetoa mafunzo kwa Wahasibu wa Wakala wa Vipimo (WMA) kutoka nchi nzima kuhusu uandaaji wa taarifa za fedha kwa kutumia Mfumo wa Uhasibu Serikalini maarufu kama MUSE.

Katika mafunzo hayo ambayo yalifanyika Morogoro Februari 19 hadi 21, washiriki pia walijengewa uelewa wa jinsi ya kujibu hoja za ukaguzi kupitia mada iliyowasilishwa na Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa WMA, CPA Christopher Mwakibinga.

Akielezea malengo ya kuandaa mafunzo hayo, Meneja Sehemu ya Fedha na Uhasibu WMA, CPA Ibrahim Mbinga alisema ni kuwawezesha Wahasibu wote wa Wakala kuwa na uelewa wa kuandaa Taarifa za Fedha za Nusu Mwaka (Interim Financial Statement) pamoja na zile za mwaka mzima.

"Huu ni Mfumo mpya serikalini ambao Wahasibu wote kutoka Taasisi za Umma wanapaswa kuutumia. Awali, ni Wahasibu wachache waliokuwa na uelewa wa kuandaa taarifa za fedha kwa kutumia Mfumo huu hivyo kazi hiyo ilikuwa inachukua muda mrefu.

Mafunzo yaliyotolewa yatarahisisha zaidi utendaji kazi kwakuwa kila mmoja sasa atakuwa na uwezo wa kuandaa taarifa za eneo lake," alifafanua.

Kuhusu faida za kutumia Mfumo wa MUSE, CPA Mbinga alibainisha kuwa ni pamoja na kupunguza gharama kwa Serikali kutokana na Taasisi zote za Umma kutumia Mfumo mmoja tofauti na awali ambapo kila Taasisi ilitumia Mfumo wake.

Aliongeza kuwa, kutumia Mfumo mmoja kumeongeza mfanano wa taarifa (uniformity) hali inayorahisisha pia uandaaji wa taarifa kubwa ya fedha ya Serikali.

CPA Mbinga alieleza faida nyingine ya kutumia Mfumo wa MUSE kuwa ni kuwezesha utunzaji wa siri za Serikali kutokana na Mfumo huo kusimamiwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao (EGA) tofauti na awali ambapo Mifumo iliyokuwa ikitumiwa na Taasisi ilikuwa chini ya usimamizi wa watu mbalimbali kutoka nje ya nchi.

Faida nyingine aliyoieleza ni kwamba Mfumo wa MUSE umezingatia viwango vya kimataifa vya uandaaji taarifa za fedha katika sekta za umma hivyo kuziwezesha Taasisi za Umma kuandaa taarifa zake kwa viwango vya kimataifa.

Akifunga mafunzo hayo, Mkurugenzi wa Huduma za Biashara, Karim Mkorehe aliwataka wahasibu wa WMA kutumia mafunzo hayo kuboresha utendaji kazi katika vituo vyao na kufanya kazi kwa weledi wakati wa kutimiza majukumu yao.

Wahasibu kutoka mikoa 31 ya kivipimo kote nchini walishiriki mafunzo hayo.



*Mkurugenzi wa Huduma za Biashara kutoka Wakala wa Vipimo (WMA), Karim Mkorehe (kushoto), akizungumza na Wahasibu kutoka mikoa 31 ya kivipimo kote nchini (hawapo pichani) baada ya kufunga mafunzo ya uandaaji wa taarifa za fedha kwa kutumia Mfumo wa Uhasibu Serikalini maarufu kama MUSE, Februari 21, 2025 mjini Morogoro.*



*Meneja Sehemu ya Fedha na Uhasibu kutoka Wakala wa Vipimo (WMA), CPA Ibrahim Mbinga, akizungumza wakati wa mafunzo kwa Wahasibu wa WMA nchi nzima kuhusu uandaaji wa taarifa za fedha kwa kutumia Mfumo wa Uhasibu Serikalini maarufu kama MUSE, Februari 21, 2025 mjini Morogoro.*











*Wahasibu kutoka mikoa 31 ya kivipimo, iliyoko chini ya Wakala wa Vipimo (WMA) nchini kote, wakifuatilia mafunzo ya uandaaji wa taarifa za fedha kwa kutumia Mfumo wa Uhasibu Serikalini maarufu kama MUSE yaliyofanyika Februari 19 hadi 21, 2025 mjini Morogoro.*

# HABARI KATIKA PICHA






*Wahasibu kutoka mikoa 31 ya kivipimo, iliyoko chini ya Wakala wa Vipimo (WMA) nchini kote, wakifuatilia mafunzo ya uandaaji wa taarifa za fedha kwa kutumia Mfumo wa Uhasibu Serikalini maarufu kama MUSE yaliyofanyika Februari 19 hadi 21, 2025 mjini Morogoro.*

# WMA PWANI YAKAGUA BIDHAA ZA VIWANDANI KUMLINDA MLAJI







*Wataalamu kutoka Wakala wa Vipimo (WMA) Mkoa wa Pwani, wakikagua bidhaa zinazozalishwa na viwanda vilivyoko mkoani humo kwa lengo la kumlinda mteja.*

**Pwani**

Wakala wa Vipimo (WMA) mkoani Pwani, wameendesha zoezi la ukaguzi wa bidhaa mbalimbali zinazozalishwa na viwanda vilivyoko mkoani humo ili kujiridhisha kama zina vipimo sahihi na hivyo haziwapunji wateja.

Akizungumza katika siku ya kwanza ya utekelezaji wa zoezi hilo, Februari 12, 2025 Kaimu Meneja wa WMA Pwani, Isaac Bilahi alisema kuwa lengo lake ni kuhakikisha bidhaa zote zinazozalishwa mkoani humo zinakidhi vigezo vilivyowekwa na Wakala kupitia Sheria ya Vipimo, Sura Namba 340.

"Miongoni mwa bidhaa tunazokagua ni pamoja na zile za chuma zinazozalishwa na viwanda vingi vilivyoko katika Mkoa wetu wa Pwani," alibainisha.

Aidha, aliongeza kuwa ukaguzi huo ulihusisha pia vipimo katika mifuko au vifungashio vya saruji.

Kufuatia zoezi hilo la ukaguzi ambalo ni sehemu ya majukumu yanayotekelezwa na WMA kote nchini, baadhi ya wakazi wa Mkoa wa Pwani waliipongeza Wakala kwa kuwajali wananchi na kuhakikisha wanapata kilicho stahiki pale wanaponunua bidhaa mbalimbali.

"Tunaomba zoezi hili liwe linafanyika mara kwa mara," walitoa wito.

WMA hufanya kaguzi za aina hiyo usiku na mchana katika maeneo mbalimbali zinakopatikana bidhaa mbalimbali zikiwemo za viwandani, kwa mawakala pamoja na kwenye magari yanayosafirisha bidhaa hizo kutoka viwandani kwenda madukani.

# BODI WMA YAKOSHWA NA UJENZI JENGO LA BIL. 6.2/-



*Jengo la Ofisi Kuu ya Wakala wa Vipimo (WMA) lililopo eneo la Medeli jijini Dodoma.*

**Dodoma**

Bodi ya Ushauri ya Wakala wa Vipimo (WMA) imekagua Jengo la Ofisi Kuu ya Wakala hiyo lililo katika hatua za mwisho kukamilika na kukiri kuridhishwa na hatua iliyofikiwa katika ujenzi.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya ziara hiyo ya ukaguzi iliyofanyika Februari 7, 2025 jijini Dodoma, Mwenyekiti wa Bodi, Prof. Eliza Mwakasangula alisema hatua iliyofikiwa katika ujenzi husika, inadhihirisha pasipo shaka kuwa litakabidhiwa katika hali ya ukamilifu kama inavyotarajiwa.

"Tumeridhishwa sana na kazi iliyofanywa na Mkandarasi kwa kushirikiana na Mshauri Elekezi. Kinachofanyika sasa ni kukamilisha kazi ndogo ndogo zilizosalia. Kwa hatua iliyofikiwa, hatuna shaka hivi karibuni Jengo litakuwa limekamilika kwa viwango stahiki," alisema.

Aidha, Prof. Mwakasangula alimshukuru Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutenga bajeti ya ujenzi wa Jengo hilo ambalo limegharimu takribani shilingi bilioni 6.2 ambazo ni fedha za ndani.

Pia, alimshukuru Waziri wa Viwanda na Biashara, Mhe. Dkt. Selemani Jafo na Menejimenti yake pamoja na kumpongeza Mtendaji Mkuu wa WMA, Alban Kihulla na Menejimenti yake yote kwa usimamizi mzuri wa jengo hilo.

Kwa upande wake, Mtendaji Mkuu Kihulla aliwaeleza waandishi wa habari kuwa kukamilika kwa jengo hilo kutatatua changamoto mbalimbali za kiofisi.

"Tumeanza na jengo hili lakini matarajio ni kujenga katika maeneo mengine ili mazingira ya kiofisi kwa wateja wanaokuja kupata huduma yawe mazuri lakini na kwa watumishi pia."

Alitaja faida nyingine ya kukamilika kwa jengo hilo kuwa ni kuwezesha vifaa vya kitaalamu kukaa katika mazingira ambayo ni mazuri ili kuendana na usahihi wa kimataifa.

Naye Mkurugenzi wa Kampuni ya Ukandarasi ya Mohamed Builders inayojenga jengo hilo, Jaffar Mohamed alimhakikishia Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi hiyo kuwa watakabidhi jengo hilo likiwa limekamilika hivi karibuni kama ilivyopangwa.

Wafanyakazi wa Wakala wa Vipimo Makao Makuu, ambao kwa sasa wako Dar es Salaam, wanatarajiwa kuhamia Dodoma baada ya kukamilika kwa Jengo hilo ikiwa ni kutimiza maelekezo ya Serikali yanayozitaka Taasisi na Mashirika yote ya Umma kuhamia Makao Makuu ya nchi, Dodoma.




Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya Wakala wa Vipimo (WMA), Prof. Eliza Mwakasangula akizungumza na Waandishi wa Habari jijini Dodoma, Februari 7, 2025 baada ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa Jengo la Ofisi Kuu ya Wakala hiyo.



Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya Wakala wa Vipimo (WMA), Prof. Eliza Mwakasangula (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya Wajumbe wa Bodi hiyo, baada ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa Jengo la Ofisi Kuu ya WMA jijini Dodoma, Februari 7, 2025.



Bodi ya Ushauri ya Wakala wa Vipimo (WMA), ikikagua maendeleo ya ujenzi wa Jengo la Ofisi Kuu ya Wakala hiyo jijini Dodoma, Februari 7, 2025.

# HABARI KATIKA PICHA







*Matukio mbalimbali wakati Bodi ya Ushauri ya Wakala wa Vipimo (WMA), ilipokagua maendeleo ya ujenzi wa Jengo la Ofisi Kuu ya Wakala hiyo jijini Dodoma, Februari 7, 2025.*







*Matukio mbalimbali wakati Bodi ya Ushauri ya Wakala wa Vipimo (WMA), ilipokagua maendeleo ya ujenzi wa Jengo la Ofisi Kuu ya Wakala hiyo jijini Dodoma, Februari 7, 2025.*







*Matukio mbalimbali wakati Bodi ya Ushauri ya Wakala wa Vipimo (WMA), ilipokagua maendeleo ya ujenzi wa Jengo la Ofisi Kuu ya Wakala hiyo jijini Dodoma, Februari 7, 2025.*







*Matukio mbalimbali wakati Bodi ya Ushauri ya Wakala wa Vipimo (WMA), ilipokagua maendeleo ya ujenzi wa Jengo la Ofisi Kuu ya Wakala hiyo jijini Dodoma, Februari 7, 2025.*

Pwani

# WANUNUZI WAKUBWA BIDHAA ZA VIWANDANI WASHAURIWA KUZIHAKIKI

Wakala wa Vipimo (WMA) Mkoa wa Pwani, imewashauri wafanyabiashara wakubwa ambao hununua bidhaa kutoka viwandani, kuzihakiki ili kujiridhisha endapo zina viwango stahiki kabla ya kuzipokea kwa ajili ya kuwauzia walaji mbalimbali.

Meneja wa WMA mkoani humo, Isaac Birahi alitoa rai hiyo Februari 27, 2025 wakati wa zoezi la utoaji elimu kwa wadau wenye maduka ya kuuzia vifaa vya ujenzi hususani bidhaa za chuma kama vile nondo.

Ili kuwezesha utekelezaji wa utaratibu huo wa kukagua bidhaa zinazotoka viwandani, Birahi aliwashauri wafanyabiashara wakubwa kuhakikisha wanakuwa na wataalamu katika ofisi zao, ambao watawajibika kufanya kazi hiyo.

Aidha, amesema kuwa WMA iko tayari kutoa elimu ya vipimo kwa wataalamu kutoka kwa wafanyabiashara hao ili kuwawezesha kukagua bidhaa hizo kwa ufanisi.

"Lengo letu ni kuhakikisha kuwa Sheria ya Vipimo, Sura Namba 340 inasimamiwa na kulindwa," alisema.

Kuhusu utaratibu wa kukagua bidhaa hizo, Birahi aliwashauri kufanya zoezi hilo kila wanaponunua bidhaa, kabla ya kuzipokea na kuzihifadhi katika maghala yao.

Akizungumza wakati wa zoezi hilo la utoaji elimu, mmoja wa washiriki aliishukuru na kuipongeza WMA kwa kuwapatia fursa ya kujifunza kuhusu vipimo.

"Kwa asilimia kubwa, elimu ya vipimo tulikuwa hatuifahamu. Leo tumejifunza na tumepewa ofa pia kwa ajili ya kujifunza Zaidi. Tunawashukuru sana WMA."

Zoezi la utoaji elimu ya vipimo ni endelevu na litaendelea kutolewa katika makundi mbalimbali. Wakala wa Vipimo Mkoa wa Pwani imetoa wito kwa wamiliki wa viwanda na maduka ya vifaa vya ujenzi kuwapeleka wataalamu wake kupata mafunzo ya upimaji wa nondo na namna ya kutumia vifaa mbalimbali vya upimaji.



*Meneja wa Wakala wa Vipimo (WMA) Mkoa wa Pwani, Isaac Birahi akitoa elimu ya vipimo kwa baadhi ya wawakilishi wa wafanyabiashara wakubwa wa bidhaa za viwandani, Februari 27, 2025.*







*Matukio mbalimbali wakati wa utoaji elimu ya vipimo kwa wafanyabiashara wakubwa wa bidhaa za viwandani mkoani Pwani, Februari 27, 2025.*

# YALIYOJIRI MACHI 25, 2025 WAKATI AFISA MTENDAJI MKUU WA WAKALA WA VIPIMO (WMA), BW. ALBAN KIHULLA AKIZUNGUMZA NA WAANDISHI WA HABARI KUHUSU MAFANIKIO NA MWELEKEO WA WMA NDANI YA UONGOZI WA SERIKALI YA AWAMU YA SITA KATIKA UKUMBI WA IDARA YA HABARI – MAELEZO, DODOMA

# Wakala imefanikiwa kuhakiki vipimo 3,668,149 vitumikavyo katika sekta mbalimbali nchini kati ya vipimo 3,923,652 ilivyopanga kuhakiki ambayo ni sawa na asilimia 94 ya lengo.

# Kati ya vipimo hivyo vilivyohakikiwa, vipimo 102,969 vilikutwa na mapungufu ambayo yalirekebishwa na kuruhusiwa kuendelea kutumika na vipimo 5,607 vilikataliwa kutumika baada ya kuonekana na mapungufu ambayo hayarekebishiki.

# Wakala inaishukuru Serikali ya Awamu ya Sita kwa kuiwezesha kupata ajira za watumishi 186 wa kada ya ukaguzi wa vipimo ambao wataongeza nguvu kwenye jukumu la uhakiki na ukaguzi wa vipimo hapa nchini.

# Wakala imejenga majengo mapya ya Ofisi katika Mkoa wa Mara na Simiyu. Vilevile, ujenzi wa ofisi hizo umefanyika katika Mkoa wa Dodoma ambapo ujenzi wa jengo ambalo sasa linatumika kama Ofisi za Wakala wa Vipimo Makao Makuu, ulikamilika Machi, 2025 kwa gharama ya shilingi bilioni 6.99.

# Wakala imeendelea kununua vifaa vya kitaalam kwa ajili ya kurahisisha utoaji wa huduma ikiwemo Iron Weight 500kg (100) kwa ajili ya kufanya uhakiki na ukaguzi wa mizani kubwa zinazotumika viwandani na kwenye barabara na mitambo mikubwa miwili na mitambo midogo 10 inayobebeka kwa ajili ya kuhakiki dira za maji.

# Wakala wa Vipimo imenunua mitambo 12 kwa ajili ya kuhakiki vipima mwendo kwenye vyombo vya usafiri. Kati ya mitambo hiyo, mitambo 10 inabebeka ambayo itasambazwa kwenye mikoa.

# Vilevile, imenunua mitambo miwili ya kusimika ambapo mtambo mmoja unaendelea kusimikwa katika kituo cha uhakiki wa vipimo Misugusugu na mtambo mwingine utasimikwa katika Ofisi ya Makao Makuu Dodoma.

# Wakala imenunua mita nne za mtiririko kwa ajili ya kuhakiki mita zilizofungwa kwenye maghala ya kuhifadhia mafuta, migodini, viwanja vya ndege na sehemu nyingine zinazotumika kujaza mafuta kwa kasi kubwa kwa lengo la kuhakikisha kuwa mita hizo zinatoa vipimo sahihi vya kiasi cha mafuta.

# Kuanzia mwaka 2021/22 hadi Februari 2025, Wakala imechangia jumla ya shilingi bilioni 17.1 kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Aidha, kwa mwaka wa fedha 2024/25, Wakala inatarajia kuchangia zaidi ya shilingi bilioni 7 ambapo kufikia Februari 2025, Wakala imechangia kiasi cha shilingi bilioni 3.8.

# Wakala imefanikiwa kuhakiki idadi kubwa ya matenki ya magari yabebayo vimiminika, shughuli ambayo inafanywa kupitia kituo kikubwa cha uhakiki wa vipimo cha Misugusugu. Kituo hicho ni moja ya vituo vya kisasa kwenye ukanda wa Afrika Mashariki na Kati ambacho kina uwezo wa kupima matenki ya malori 60 kwa siku.

# Kituo cha Misugusugu kimefanikiwa kuhakiki tenki 21,746 ambapo ndiyo hutumika kusafirisha shehena ya vimiminika kutoka bandari ya Dar es Salaam na kwenda mikoani au nchi za nje kama vile Zambia, Rwanda, Malawi, Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

# Wakala wa Vipimo inaendelea kutoa huduma za uhakiki wa kiasi cha mafuta (jamii ya petroli na mafuta ya kula) yanayoingia nchini kupitia bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara. WMA imefanikiwa kuhakiki jumla ya lita 30,645,930,571 za mafuta kwa meli 546 zilizowasili nchini.

# Maboresho hayo yalijumuisha kusimika mita ya kisasa katika bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara na kupelekea kuongezeka kwa ujazo wa mafuta yaliyohakikiwa kufikia jumla ya lita 30,645,930,571 ambapo kati yake, lita 13,888,897,421 kwa ajili ya matumizi ya ndani na lita 16,757,033,150 zilisafirishwa nje ya nchi.

INAENDELEA UK. 21




*Afisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Vipimo (WMA), Alban Kihulla akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mafanikio na mwelekeo wa WMA katika kipindi cha Uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita, Ukumbi wa Idara ya Habari - MAELEZO, Dodoma.*

# YALIYOJIRI MACHI 25, 2025 WAKATI AFISA MTENDAJI MKUU WA WAKALA WA VIPIMO (WMA), BW. ALBAN KIHULLA AKIZUNGUMZA NA WAANDISHI WA HABARI KUHUSU MAFANIKIO NA MWELEKEO WA WMA NDANI YA UONGOZI WA SERIKALI YA AWAMU YA SITA KATIKA UKUMBI WA IDARA YA HABARI – MAELEZO, DODOMA

INATOKA UK. 20

# Wakala imehakiki kiasi cha gesi iliyoingia nchini kwa njia ya Meli ambapo jumla ya tani za ujazo 958,593.17 za gesi zilishishwa na Meli 210 zilizowasili nchini.

# Katika kuunga mkono kampeni ya matumizi ya nishati safi ya kupikia, Wakala inafanya ukaguzi na uhakiki wa vipimo kwenye mitungi ya gesi ili kuhakikisha kuwa wanunuzi wa gesi wanapata kiasi sahihi kulingana na thamani ya fedha wanayolipa kwa ajili ya huduma hiyo.

# Wakala imepatiwa jumla ya magari 21 ili kutekeleza kwa ufasaha kazi za uhakiki na ukaguzi wa vipimo katika maeneo mbalimbali nchi nzima, magari hayo pia yamewezesha utunzaji mzuri wa vifaa vya kitaalam.

# Wakala imefanikiwa kufungua vituo maalum 10 katika mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Kilimanjaro, Songwe, Mbeya, Kagera, Kigoma na Mara kwa ajili ya kukagua bidhaa zote zinazozalishwa ndani ya nchi na zile zinazoingiza kutoka nje ya nchi.

# Jumla ya bidhaa 70,660 zilizoingia nchini zilikaguliwa. Wakala inatarajia kuanza uhakiki wa Taxi Meter ambapo imeshanunua mitambo 12, miwili ya kusimika ambapo mtambo mmoja unaendelea kusimikwa katika Kituo cha Uhakiki wa Vipimo Misugusugu na mtambo mwingine utasimikwa katika Ofisi ya Makao Makuu Dodoma.

# Vilevile, mitambo mingine 10 (portable taximeter) itagawiwa kwenye mikoa kwa ajili ya kuhakiki vipima mwendo kwenye vyombo vya usafiri.

# Wakala imejipanga kuendelea kufungua Ofisi sehemu mbalimbali zinazoonekana kuwa na ukuaji wa shughuli za kiuchumi na kijamii ili kuendelea kuwalinda watoa huduma na wapokea huduma kupitia matumizi ya vipimo vilivyohakikiwa.

# Wakala itaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusiana na matumizi sahihi ya vipimo kwa kutumia vyombo vya habari, mitandao ya kijamii pamoja na kushiriki kwenye maonesho na makongamano mbalimbali ili wananchi wazidi kufahamu Wakala wa Vipimo, majukumu yake na umuhimu wa kutumia vipimo sahihi.

**IMEANDALIWA NA IDARA YA HABARI - MAELEZO**




*Afisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Vipimo (WMA), Alban Kihulla akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mafanikio na mwelekeo wa WMA katika kipindi cha Uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita, Ukumbi wa Idara ya Habari - MAELEZO, Dodoma.*

Mbiu ya

# VIPIMO

JARIDA LA WAKALA WA VIPIMO




## MAWASILIANO:


Wakala wa Vipimo (WMA)
Jengo la NSSF (Mafao), S.L.P 313, Dar es Salaam.

wakalawavipimotanzania

0800110097

www.wma.go.tz